

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



S.L.P 1951  
Moshi

**TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI**

**KILIMANJARO APRIL 28, 2020**

**DIWANI WA KATA YA MPINJI WILAYA YA SAME NA MMILIKI WA  
KAMPUNI YA E. G. MHINA ELECTRICAL SERVICES KUFIKISHWA  
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI SAME KWA UTAPELI**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoani Kilimanjaro kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, inatarajia kuwafikisha katika Mahakama ya Wilaya ya Same watuhumiwa wawili akiwemo Diwani wa Kata ya Mpinji Ndugu ASTON MGONJA na Ndugu EMILY GREYSON MHINA ambaye ni mmiliki wa kampuni ya E.G MHINA ELECTRICAL SERVICES.

Ndugu ASTON MGONJA, anatuhumiwa kujipatia fedha kiasi cha shilingi milioni tatu (3,000,000/=) kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa SIFA ARON KITUNGA, akimrubuni kwamba ana uwezo wa kumsaidia kupata kibali cha kumiliki Duka la Madawa Muhimu pamoja na Zahanati baada ya duka lake kufungiwa hapo awali na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Same kwa kutokuwa na kibali.

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Kilimanjaro ulibaini kuwa Mtuhumiwa alijipatia fedha hizo huku akijua kwamba hana uwezo wa kumsaidia Sifa Aaron Kitunga kupata kibali hicho. Mtuhumiwa alitenda kosa hilo tarehe 04/06/2018. Uchunguzi dhidi ya tuhuma hii umekamilika na mtuhumiwa atafikishwa mahakamani wakati wowote kuanzia sasa.

Ndugu EMILY GREYSON MHINA ambaye ni fundi umeme na mmiliki wa kampuni ya E.G MHINA ELECTRICAL SERVICES yeye anakabiliwa na kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa wananchi wa kijiji cha GUNDUSINE kilichopo Wilayani Same, akiwalaghai wananchi hao kuwa TANESCO Wilaya ya Same wapo kwenye mchakato wa kupeleka umeme wa REA vijijini, ikiwa ni pamoja na kijiji hicho, maelezo ambayo yalikuwa ya uongo. Mtuhumiwa alijipatia kiasi cha shilingi elfu thelathini na tano (sh 35,000/=) kutoka kwa kila kaya na kufanikiwa kukusanya jumla ya sh. 2,065,000/= kutoka kwa kaya 59. Fedha hizo alizikusanya kupitia kwa Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mbukwe.

Mtuhumiwa alipokea fedha hizo akidai kuwa ni gharama za ramani na muhuri na pia aliwajazia fomu za TANESCO za "application and Agreement for power Supply" akionyesha kuwa nyumba za wateja hao zimefanyiwa "wiring" wakati sio kweli.

Mtuhumiwa alitenda kosa hilo kati ya mwezi Novemba 2011 na Januari 2018 na mpaka leo kazi hiyo haijafanyika. Vilevile TANESCO Same hawakuwa na mapendekezo wala utekelezaji wa mradi wa REA vijijini katika kijiji hicho. Uchunguzi umekamilika na mtuhumiwa atafikishwa mahakamani wakati wowote kuanzia sasa.

Nitoe rai kwa wananchi wote kujihadhari na matapeli.

Imetolewa na,  
Fidelis Kalungura

**Mkuu wa TAKUKURU (M)**  
**KILIMANJARO**